# Serikali yawashukia Maofisa Uvuvi

Na Mbaraka Kambona

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul amesema hakuna haja ya kuendelea kuwa na Maofisa Uvuvi ambao wanashirikiana na wahalifu, kufanya vitendo vya hujuma wakati kuna vijana wengi wenye nia njema ya kulitumikia taifa wanahangaika na ajira.

Aliyasema hayo alipotembelea kiwanda cha kuchakata samaki, Alpha kilichopo Vingunguti jijini Dar es Salaam juzi.

Kwa mujibu wa Gekul, sehemu kubwa ya upungufu wa rasilimali za uvuvi unachangiwa na baadhi ya Maofisa Uvuvi, wasiokuwa waaminifu ambao wamekuwa wakishirikiana na wahalifu kufanya uvuvi usioendelevu unaosababisha kupungua kwa samaki.

"Tulikuwa Kanda ya Ziwa na hapa pia, kilio ni hicho hicho malighafi, malighafi zinapungua kwa sababu baadhi ya Maofisa Uvuvi wanashiriki katika vitendo vya uvuvi haramu, wanashirikiana na wahalifu, hata pale ambapo vyombo vya ulinzi na usalama vinapotaka kufanya operesheni ya kuwakamata wahalifu, wamekuwa wakitoa taarifa kwa wahalifu hao kama ambavyo ilitokea hivi karibuni kule wilayani Babati," alisema.

Aliongeza; "Kwa nini tuendelee na watu wa namna hii wakati kuna vijana wengi wenye nia njema na taifa lao wapo huko nje, hawana ajira na huku ndani ya serikali kuna baadhi ya watu wanahujumu taifa na uchumi wa nchi, hatuna haja kuendelea kuwa na watu kama hawa," alisisitiza Gekul.

Alisema itakuwa aibu wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza hapa nchini, halafu washindwe kuendelea na uzalishaji kwa kukosa malighafi kutokana na kushindwa kudhibiti uvuvi haramu.

Naibu Waziri huyo alisema, wawekezaji ni muhimu kwa uchumi wa taifa kwa sababu wanalipa kodi na tozo mbalimbali ambazo zinasaidia kukuza pato la taifa, uchumi wa nchi na kutoa ajira kwa vijana.

Aliwataka maofisa hao, ambao wanaojihusisha na vitendo hivyo kujirekebisha na washirikiane kwa karibu na vyombo vya ulinzi na usalama, ili kwa pamoja waweze kukomesha vitendo hivyo kwa lengo la kunusuru rasilimali za uvuvi.

"Tutimize wajibu wetu tukijuwa kuwa uvuvi haramu ukiendelea, tutaviua hivi viwanda na matokeo yake ajira nazo kwa vijana wetu zitapotea," alisema.

Naibu Waziri huyo, aliwataka Maofisa Uvuvi wote nchini kuendelea kuchukua hatua za haraka kudhibiti hali iliyopo ya upotevu wa rasilimali za uvuvi katika maeneo yote yalipo maji na maziwa.

Awali Meneja wa Uzalishaji wa Kiwanda cha Alpha, Sreejish Srinivasan wakati akitoa taarifa ya uzalishaji wa kiwanda hicho, alisema changamoto kubwa wanayokumbana nayo ni uchache wa malighafi kwa ajili ya kuchakatwa kiwandani hapo na mpaka sasa, wanafanya shughuli zao chini ya asilimia 15 ya uwezo wa kiwanda



Scanned with CamScanner

hayo wakati wa kikao chake

apate huduma za serikali mahali popote alipo, badala ya kufuata

MAJIRA UK 9

matumia fedha nyingi kununua mifumo ya TEHAMA nje ya nchi, hivyo anataka wabunifu wa

Yonazi alimshukuru waziri kwa kikao hicho na kuongeza ari kwa wafanyakazi kutumikia wananchi.

nemu limali aadhi uwa uwa fanya bisha

a na icho gua ofisa ndo iana apo ama ni ya uwa hao buni

elee kuna a na vana una aifa naja ma

zaji za we sa wa

na, mi pa zo fa, wa

ao yo wa na ze va vi. va a,



**Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (kulia) akikagua moja ya nyavu inayozalishwa katika kiwanda cha kutengeneza nyavu za kuvulia samaki Nyamagara kilichopo Chanika jijini Dar es Salaam alipokitembelea juzi.** (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner

# Gekul 'awashukia' maofisa uvuvi wanaoshirikiana wahalifu

**Na Mbaraka Kambona**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, amesema hakuna haja ya kuendelea kuwa na maofisa uvuvi wanaoshirikiana na wahalifu kufanya vitendo vya hujuma wakati kuna vijana wengi wenye nia njema ya kulitumikia taifa wanahangaika na ajira.

Gekul aliyasema hayo alipotembelea kiwanda cha kuchakata samaki Alpha, kilichopo Vingunguti, jijini Dar es Salaam juzi

Kwa mujibu wa Gekul sehemu kubwa ya upungufu wa rasilimali za uvuvi unachangiwa na baadhi ya maofisa uvuvi ambao sio waaminifu wanaoshirikiana na wahalifu kufanya uvuvi usioendelevu unaosababisha kupungua kwa samaki.

"Tulikuwa Kanda ya Ziwa na hapa pia kilio ni hicho hicho malighafi, malighafi zinapungua kwa sababu baadhi ya maofisa uvuvi wanashiriki katika vitendo vya uvuvi haramu, wanashirikiana na wahalifu, hata pale ambapo vyombo vya ulinzi na usalama vinapotaka kufanya operesheni ya kuwakamata wamekuwa wakitoa taarifa kwa wahalifu hao kama ambavyo ilitokea hivi karibuni kule wilayani Babati," alisema Gekul. "Kwanini tuendelee na watu wa namna hii wakati kuna vijana wengi wenye nia njema na taifa lao wapo huko nje hawana ajira na huku ndani ya serikali kuna baadhi ya watu wanahujumu taifa na uchumi wa nchi, hatuna haja kuendelea kuwa na watu kama hawa," alisisitiza Gekul.

Alisema kuwa itakuwa aibu wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza nchini halafu washindwe kuendelea na uzalishaji kwa kukosa malighafi kutokana na kushindwa kudhibiti uvuvi haramu.


Aliongeza kuwa wawekezaji ni muhimu kwa uchumi wa taifa kwa sababu wanalipa kodi na tozo mbalimbali ambazo zinasaidia kukuza pato la taifa, uchumi wa nchi na kutoa ajira kwa vijana.

Aliwataka maofisa wanaojihusisha na vitendo hivyo kujirekebisha na washirikiane kwa karibu na vyombo vya ulinzi na usalama ili kwa pamoja waweze kukomesha vitendo hivyo kunusuru rasilimali za uvuvi.

"Tutimize wajibu wetu tukijuwa kuwa uvuvi haramu ukiendelea tutaviua hivi viwanda na matokeo yake ajira nazo kwa vijana wetu zitapotea," alieleza Gekul.

Aliwataka maofisa uvuvi wote nchini kuendelea kuchukua hatua za haraka kudhibiti hali iliyopo ya upotevu wa rasilimali za uvuvi katika maeneo yote yalipo maji na maziwa.

Awali, Meneja wa Uzalishaji wa Kiwanda cha Alpha, Sreejish Srinivasan, akitoa taarifa ya uzalishaji wa kiwanda hicho alieleza kuwa changamoto kubwa wanayokumbana nayo ni uchache wa malighafi kwa ajili ya kuchakatwa kiwandani hapo na mpaka sasa wanafanya shughuli zao chini ya asilimia 15 ya uwezo wa kiwanda hicho.



Wafanyakazi wa kiwanda cha kuchakata samaki Alpha, wakimwonyesha Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (wa kwanza kulia), minofu ya samaki aina ya pweza ambayo imechakatwa katika kiwanda hicho, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

TAKUKURU yafikisha wanane mahakamani

mawasiliano serikalini cha wizara hiyo, Dk Ndugulile aliyasema hayo wakati wa kikao na wafanyakazi wa wizara yake kilicho-

muumini wa michakato, anahitaji kuona matokeo ili kuhakikisha Tehama inatumika kujibu changamato za wananchi ili wapate

wizara hiyo mpya.

Kwa upande wale, Dk Yonazi alimshukuru Dk Ndugulile kwa kikao hicho alichosema kitaongeza ari ya wafanyakazi kutumikia

kazi kwa ushirikiano, kujituma na kushirikiana na menejimenti kwenye kushauri yapi yafanyike katika nyanja ya Tehama ili kukuza uchumi wa taifa.

wafuate utaratibu halali uliowekwa kisheria ikiwamo kupata kibali kutoka ofisi ya misitu na kuepuka uharibifu wa mazingira," alisema.

HABARILEO UK 15.

# Gekul awaonya maofisa uvuvi wanaohujumu sekta

**Na Mwandishi Maalumu**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul amesema hakuna haja kuendelea kuwa na maofisa uvuvi wanaoshirikiana na wahalifu kuhujumu sekta hiyo wakati kuna vijana wengi wenye nia njema ya kulitumikia Taifa wanahangaika kupata ajira.

Naibu Waziri huyo alitoa onyo hilo alipotembelea kiwanda cha kuchakata samaki cha Alpha kilichopo Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana.

"Tulikuwa Kanda ya Ziwa na hapa pia kilio ni hicho hicho malighafi, malighafi zinapungua kwa sababu baadhi ya maofisa uvuvi wanashiriki katika vitendo vya uvuvi haramu, wanashirikiana na wahalifu hata pale ambapo vyombo vya ulinzi na usalama vinapotaka kufanya operesheni ya kuwakamata wahalifu wamekuwa wakitoa taarifa kwa wahalifu hao kama ambavyo ilitokea hivi karibuni kule wilayani Babati," alisema.

Kwa mujibu wa Gekul, sehemu kubwa ya upungufu wa rasilimali za uvuvi inachangiwa na baadhi ya maofisa uvuvi ambao si waaminifu na wamekuwa wakishirikiana na wahalifu kufanya uvuvi usio endelevu hivyo kusababisha kupungua kwa samaki.

"Kwa nini tuendelee na watu wa namna hii wakati kuna vijana wengi wenye nia njema na taifa lao wapo huko nje hawana ajira na huku ndani ya serikali kuna baadhi ya watu wanahujumu taifa na uchumi wa nchi hatuna haja kuendelea kuwa na watu kama hawa."

"Itakuwa aibu wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza hapa nchini halafu washindwe kuendelea na uzalishaji kwa kukosa malighafi kutokana na kushindwa kudhibiti uvuvi haramu," alisema.

Gekul alisema wawekezaji ni muhimu kwa uchumi wa taifa kwa sababu wanalipa kodi na tozo mbalimbali ambazo zinasaidia kukuza pato la taifa, uchumi wa nchi na kutoa ajira kwa vijana.

Aliwataka maofisa wanaojihusisha na vitendo hivyo kujirekebisha na washirikiane kwa karibu na vyombo vya ulinzi na usalama ili kwa pamoja wakomeshe vitendo hivyo kwa lengo la kunusuru rasilimali za uvuvi.

"Tutimize wajibu wetu tukijuwa kuwa uvuvi haramu ukiendelea tutaviua hivi viwanda na matokeo yake ajira nazo kwa vijana wetu zitapotea," alisema.

Scanned with CamScanner

ya vitega uchumi ya Micheweni na Maziwangombe, ambapo pia aliwaeleza wananchi kwamba fursa za ajira zitakapoanza katika

ili kufikia malengo yaliyokusudi wa ya kurahisisha uwekezaji na kuitaka wizara husika kupanga na kutenga fedha kwa ajili ya

kanaji wa ajira zikiwamo 300,000 zilizoelezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020-2025.

Dk Mwinyi kwa uamuzi wake wa kuijenga barabara hiyo na kueleza kwamba wananchi wamefarajika.

HABARI LEO UK 17.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul akikagua moja ya nyavu inayozalishwa katika Kiwanda cha kutengeneza nyavu za kuvulia Samaki cha Nyamagara kilichopo Chanika, jijini Dar es Salaam alipofanya ziara ya kikazi juzi. (Na Mpigapicha Wetu).

Scanned with CamScanner



**WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho (katikati), akikata utepe kupokea kivuko cha MV.Chato II HAPA KAZI TU, katika bandari ya Kalema. Wilaya ya Chato, mkoani Geita, juzi. Ujenzi wa kivuko hicho chenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 100 za mizigo, umegharimu sh. bilioni 3.1, kitatoa huduma kati ya Chato Mharamba, Nkome na visiwa jirani vya Senga, Bukondo na Izumacheli.** (Picha na Wizara ya Ujenzi).

UHURU UK9.

# Maofisa uvuvi wawekwa kikaangoni

**Na Mbaraka Kambona**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, amesema hakuna haja ya kuendelea kuwa na maofisa uvuvi wanaoshirikiana na wahalifu kufanya vitendo vya hujuma, wakati kuna vijana wengi wenye nia njema ya kulitumikia Taifa wanahangaika na ajira.

Gekul, aliyasema hayo juzi, alipotembelea kiwanda cha kuchakata samaki cha Alpha, kilichoko Vingunguti, Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Gekul, sehemu kubwa ya upungufu wa rasilimali za uvuvi unachangiwa na baadhi ya maofisa uvuvi, ambao siyo waaminifu, wamekuwa wakishirikiana na wahalifu kufanya uvuvi usio endelevu, unaosababisha kupungua kwa samaki.

"Tulikuwa Kanda ya Ziwa na hapa pia kilio ni hicho hicho cha malighafi kwamba zinapungua kwa sababu baadhi ya maofisa uvuvi wanashiriki katika vitendo vya uvuvi haramu, wanashirikiana na wahalifu. Hata pale ambapo vyombo vya ulinzi na usalama vinapotaka kufanya operesheni ya kuwakamata wahalifu, wamekuwa wakitoa taarifa kwa wahalifu hao kama ambavyo ilitokea hivi karibuni kule wilayani Babati," alisema.

> **Kwa nini tuendelee na watu wa namna hii wakati kuna vijana wengi wenye nia njema na taifa lao, wapo huko nje, hawana ajira na huku ndani ya serikali kuna baadhi ya watu wanahujumu taifa ...**
>
> Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul

Aliongeza: "Kwa nini tuendelee na watu wa namna hii wakati kuna vijana wengi wenye nia njema na taifa lao, wapo huko nje, hawana ajira na huku ndani ya serikali kuna baadhi ya watu wanahujumu taifa na uchumi wa nchi, hatuna haja kuendelea kuwa na watu kama hawa."

Alisema itakuwa aibu wawekezaji wanakaribishwa kuwekeza nchini, halafu washindwe kuendelea na uzalishaji kwa kukosa malighafi kutokana na kushindwa kudhibiti uvuvi haramu.

Alisema wawekezaji ni muhimu kwa uchumi wa taifa kwa sababu wanalipa kodi na tozo mbalimbali, ambazo zinasaidia kukuza pato la taifa, uchumi wa nchi na kutoa ajira kwa vijana.

Aidha, aliwataka maofisa wanaojihusisha na vitendo hivyo, kujirekebisha na washirikiane kwa karibu na vyombo vya ulinzi na usalama ili kwa pamoja wakomeshe vitendo hivyo, kwa lengo la kunusuru rasilimali za uvuvi.

"Tutimize wajibu wetu tukijuwa kuwa uvuvi haramu ukiendelea, tutaviua hivi viwanda na matokeo yake ajira nazo kwa vijana wetu zitapotea," alieleza.

Aliwataka maofisa uvuvi kote nchini, kuendelea kuchukua hatua za haraka kudhibiti hali iliyopo ya upotevu wa rasilimali za uvuvi katika maeneo yalipo maji na maziwa.

Scanned with CamScanner

UHURU

moto

# nu
# ma

lama wa nchi
za maudhui
kupunguza
go la kukuza
a Mhandisi

wa USCAF,
iona eneo la
a wa Simiyu
kupiga na
dani ya miezi
mekwisha.
aa vichache
huduma ya
hilo, hivyo
ni za simu za
iano licha ya
kuwepo.
ariadi, Festo
ya habari
mifumo ya
na za kiafya,
kuhakikisha
mawasiliano

wa kuwepo
enye taasisi
, hospitali,
sanyaji wa
kwa sasa



# Operesheni bucha za nyama zinazo kiuka taratibu yashika kasi Dar

**Na ASHURA ASSAD**

BODI ya Nyama nchini imesema oparesheni inayoendelea katika mkoa wa Dar es Salaam, kukagua maduka ya nyama ili kubaini yasiyofuata masharti ya uuzaji nyama safi na salama, inalenga kuhakikisha afya ya mlaji inazingatiwa.

Imesema yatakayobainika kutokidhi vigezo, yatachukuliwa hatua, baada ya kupewa elimu na muda wa kutosha kushughulikia changamoto zinazokiuka miongozo na taratibu za biashara hiyo.

Akizungumza na Uhuru, juzi, Kaimu Msajili wa bodi hiyo, Imani Sichwale, alisema miongoni mwa mambo yanayotakiwa kutekelezwa ni maduka ya nyama kutotumia nondo za chuma na magogo, badala yake kuweka vifaa elekezi vilivyoelekezwa na bodi hiyo.

Sichwale, alisema kwa wamiliki wataoshindwa kutekeleza matakwa yaliyoelekezwa, timu ya bodi itakapofika kwenye duka husika, itachukua hatua, ikiwamo kuondoka na vifaa vinavyotumika kinyume cha sheria na kutoa adhabu ya faini hadi mara mbili ya ile iliyopaswa kulipwa kwanza, ingawa hiyo itakuwa ni katika mazingira maalumu.

Alifafanua kuwa wafanyabiashara wanatakiwa kufuata maelekezo wanayopewa na bodi husika na kuacha kushindana na mamlaka, badala yake watii sheria bila shuruti kwa lengo la kukuza biashara zao na ustawi wa maendeleo ya jamii.

"Baadhi ya wamiliki wa maduka ya nyama ni wabishi, tumekuwa tukitoa elimu hii tangu Oktoba, mwaka jana na kuanza ukaguzi ilipofikia Desemba, mwaka jana, lakini ukifika kwenye maduka hayo unakuta lawama zisizo na msingi.

"Mara mashine zinatumia umeme mwingi, vifaa vya aluminiam havipatikani, madai hayo yote ni uongo, mashine za nyama zinatumia umeme mdogo na vifaa vya aluminiam vinapatika hadi Kariakoo, wanatakiwa wabadilike kwa kutii sheria bila shuruti,"alisema.

Kwa mujibu wa Sichwale, bodi imewaunganisha wamiliki wa maduka ya nyama na kampuni ya Water Trans, inayozalisha vifaa hivyo vya aluminiam kwa ajili ya maduka ya nyama ili kuwarahisishia upatikanaji wake.

Hata hivyo, alieleza kuwa kama wamiliki wa maduka ya nyama hawatakuwa na uwezo, wameruhusiwa kukopa na kulipa kidogo kidogo bila masharti magumu, lengo likiwa biashara zao ziendelee kwa ustawi wa pato la familia na taifa kwa ujumla.

"Ukaguzi huu ni endelevu kwa mikoa yote, tumeanzia Dar es Salaam, lengo ni kutoa elimu na kuondoa maduka ya nyama yasiyofaa katika jamii, ambayo yanasababisha kuwepo nyama isiyokuwa na ubora unaotakiwa kiafya,"alisema.

# elimu bila malipo

Scanned with CamScanner

MWANANCHI UK 2.

ka UCSAF

nifu



'Ninawaelekeza wenzetu kwamba majukumu yazingiatie utekele-zaji wa ilani ya CCM na maelekezo yaliyotolewa kwenye hotuba ya Rais wakati wa kuzindua Bunge.'

**Faustine Ndugulile**

# PICHA YA SIKU: NYAVU ZINATENGENEZWA HAPA

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (kulia) akiangalia nyavu zinazozalishwa katika Kiwanda cha kutengeneza nyavu za kuvulia Samaki cha Nyamagara kilichopo Chanika, jijini Dar es Salaam alipotembelea kiwandani hapo juzi. **Na Mpiga Picha Wetu**



wizara hiyo lakini kinyume chache watu wataishia njiani. **(Habel Chidawali)**

MWANANCHI UK 8

## Gekul awashukia maofisa uvuvi

**Dar es Salaam.** Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul amesema hakuna haja ya kuendelea kuwa na maofisa uvuvi wanaoshirikiana na wahalifu kufanya vitendo vya hujuma wakati kuna vijana wengi wenye nia njema ya kulitumikia Taifa wanahangaika na ajira.

Gekul alisema hayo juzi alipotembelea kiwanda cha kuchakata samaki cha Alpha kilichopo Vingunguti jijini Dar es Salaam.

"Tulikuwa kanda ya ziwa, kuna kilio ni hikihiki, sasa na hapa pia, malighafi zinapungua kwa sababu baadhi ya maofisa uvuvi wanashiriki vitendo vya uvuvi haramu, wanashirikiana na wahalifu, hata pale ambapo vyombo vya ulinzi na usalama vinapotaka kufanya operesheni ya kuwakamata wahalifu wao wanatoa taarifa kwa wahalifu," alisema Gekul.

Awali, Meneja wa Uzalishaji wa Kiwanda cha Alpha, Sreejish Srinivasan alisema changamoto kubwa wanayokumbana nayo ni uchache wa malighafi kwa ajili ya kuchakatwa kiwandani.

**(Elizaberth Edward)**

Scanned with CamScanner

# DC: Wafugaji leteni maziwa ya kutosha



**Njombe.** Wafugaji ng'ombe wanaopeleka maziwa Kiwanda cha Maziwa Njombe (Njolifa) wametakiwa kushikamana ili kiwanda hicho kipate maziwa ya kutosha na wao wapngeze tija.

Kauli hiyo ilitolewa na mkuu wa Wilaya ya Njombe, Ruth Msafiri kwenye mkutano maalum wa chama cha wafugaji mkoa wa Njombe uliokuwa kupendekeza jina la Njolifa kuwa Chama Kikuu cha Ushirika wa maziwa mkoani hapa.

Amesema wafugaji waungane kukifanya kiwanda hicho kiendelee kwa kupata maziwa bora na ya kutosha. Vilevile, amewataka kuzingatia katiba yao ili kuepuka migogoro.

"Tudumishe Njolifa kwa kuleta maziwa ya kutosha kusudi kiwanda chetu kitengeneze faida na kuwa na fedha ya kutosha kuwalipa wafugaji kwa wakati," Alisema Ruth.

Ofisa ushirika Halmashauri ya Njombe, Harrison Nyambo amesema kupandishwa hadhi kwa Njolifa kunatanua wigo kwa wafugaji kukisaidia kiwanda kusindika maziwa mengi zaidi na wao kukuza kipato chao.

Baadhi ya wafugaji akiwamo Ostera Mkongwa ameunga mkono mabadiliko hayo kwa kuwa chama hicho kitawasaidia kudai haki zao kutokana na madeni wanayokidai kiwanda cha Maziwa Njombe.

"Tunadai kwa muda mrefu na hatulipwi mpaka hivi sasa tunakuja kwenye kikao wenzetu wanajua tumekuja kuzungumzia masuala ya kupata hela lakini tutakaporudi tutazungumzia habari nyingine," amesema Ostera.

Meneja wa kiwanda hicho, Shahibu Himiri amesema jitihada zinaendelea kuwalipa wafugaji.

Baada ya kuwa chama kikuu cha maziwa Mkoa wa Njombe (Njolifa), Nazareth kimekuwa chama cha msingi.

**(Seif Jumanne)**

Scanned with CamScanner

MWANACHI UK 20.

## DAGAA

Mchuuzi wa dagaa, Penina Joseph akianika dagaa katika Mtaa wa Mswahili jijini Mwanza juzi ikiwa ni maandalizi kabla ya kuwauza kwa wateja wake. Ndoo moja ya dagaa wakavu inauzwa Sh 15,000 katika eneo hilo. **Picha na Mgongo kaitira**



Scanned with CamScanner